Mafundisho ya Biblia kuhusu Mateso

TAFADHALI BIBLIA YAKO IWE IMEFUNGULIWA NA UJARIBU KUTAFUTA KUMBUKUMBU REJEA ZOTE.

Ni muhimu kwamba tayari umekwisha kujifunza masomo yanayohusu Uwoga, tumaini, Imani na Sala kwa sababu mambo uliyojifunza yatakusaidia kulielewa somo hili.

Mateso ni tatizo katika maisha linaloweza kumuathiri kila mtu. Mtoto anazaliwa kipofu au mlemavu na tunauliza "Imekuwaje"? mtoto hajafanya makosa yoyote. Wanaume na Wanawake, Vijana kwa Wazee, Matajiri na Masikini wanataabika kutokana na maumivu ya magonjwa ya kukatisha tamaa ambayo mwisho wake ni kifo. Kwa nini wapate mateso?.

Adhabu kali na kifo vimepenyezwa kwa mamilioni ya watu wasio na msaada na mtu mwenye mabavu na uharibifu wa Jamii ya kisasa. Maisha yamepotea kutokana na vitendo vya ugaidi na makosa ya jinai. Mara nyingi zimekuwepo vurugu katika historia yote ya dunia, lakini, pamoja na idadi kubwa ya watu na ongezeko la uwezo wa kuharibu leo kiwango cha majanga (maafa) mara nyingi ni cha kutisha. Watu huuliza "Kwa nini Mungu anaruhusu mambo haya kutokea"?.

Swali hili aghalabu linakubali kwamba Mungu yuko na inatarajiwa kwamba Mungu daima anatenda katika wema. Kinachoangaliwa kabisa ni sababu za mateso katika dunia. Sababu hii inaweza kujumuishwa kama ifuatavyo:-

1. Katika Edeni, Mwanadamu alichagua kwenda njia yake kuliko njia ya Mungu na kujiletea ahadi ya adhabu ya kifo. Hata hivyo hii ilikuwa ni sehemu tu ya adhabu tazama kitabu cha Mwanzo kifungu cha 3 mistari ya 16 haadi 19. Maisha ya Mwanaume na Mwanamke wa Kwanza yalianza kuwa magumu sana.
2. Kwa sehemu kubwa mateso ya wanaume na wanawake ni matokeo ya ukatili wa watu wengine. Tangu mauaji ya kwanza Kaini alipomuua ndugu yake Abeli, Biblia imeorodhesha Vita, hofu kuu, mauaji na udanganyifu. Kwa jambo lolote ambalo tumelieleza kwa kuwa kwa kila tendo la ukatili kuna jukumu la mabaya litafuata. Matokeo yake hayakwepeki. Hii ni sheria rahisi ya Tendo na matokeo. Nyongeza kwa hili ni matendo ya kizazi kimoja yanavyoleta maafa kwa kizazi kinachofuata. Vitu kama siraha za sumu, ambazo huiharibu ardhi, bahari hata yamkini kizazi cha watu kwa kuwasababishia ulemavu, kuharibu (macho) uwezo wa kuona, kusikia au uwezo wa kutembea, haya yanasababishwa na watu. Mateso tuliyojiletea sisi wenyewe hatuwezi kumhusisha Mungu. Mikataba yote ya nchi ya kuzuia kutengeneza mabomu na siraha za maangamizi zilizokuwa zimewekwa tayari na majeshi wakisubiri amri kutoka kwa Serikali ya Kibinadamu.
3. Mwanadamu anaishi katika Ulimwengu unaodhibitiwa na sheria za fizikia zinazoonekana za asili na zisizokuwa za asili. Kisababishi na matokeo yake ni ya kawaida kwa mazingira yetu na maafa makubwa ya asili kama Volkano, Matetemeko, Mawimbi ya baharini, Ukame na Mafuriko yanayoleta mateso yasiyoweza kusemekana kwa wanadamu bila ya uchaguzi.

Iwapo tunafikiri kwamba Mungu ndiye anazielekeza nguvu hizi kubwa, je tunamtaka yeye kwa namna moja na nyingine atumie uwezo wake wakuchagua ambapo watu wabaya tu ndiyo watauawa na watu wazuri watanusurika?.

Katika Injili ya Luka kuna maandiko kuhusu Yesu alipoulizwa juu ya uhusiano kati ya dhambi na mateso. Utayakuta haya katika sura ya 13 mistari ya 1 hadi 5. Fundisho la Yesu ni la wazi na la kueleweka hata leo kwetu sisi. Maafa hayawatafuti wale wenye dhambi na kuwapata wenyewe tu. Mambo haya sio matokeo ya dhambi. Utendaji kazi mbaya au pengine tetemeko la ardhi, katika kisa cha mnara wa Siloam na utawala wa ukatili na wa kutisha wa Kirumi katika matukio ya wale waliouawa katika Sinagogi. Yesu ni mwangalifu kutaja sawia kwamba wajibu wa mtu mbele ya Mungu siyo kujenga hisia za uchawi katika matukio kama hayo ,lakini badala yake yanakuonya na mtu afahamu kwamba maisha ya mwanadamu kuwa ni mafupi na toba na ubatizo usiahirishwe kwa siku nyingine kwa sababu inawezekana isiwepo siku nyingine kwetu sisi.

Sasa nataka kugeukia suala lingine la mateso. Mithali sura ya 3 mistari ya 11 na 12 inatuambia kwamba yatakuwepo majaribu katika maisha kwa wale ambao ni waaminifu. Hii ni kwa sababu Mungu anawapenda na kwamba huwarudi kama ilivyo watoto katika familia aghalabu hurudiwa na baba au mama anavyowachunga na anataka wafundishwe vizuri kwa maisha ya baadaye. Kurudiwa ambako katika somo hili neno lingine ni mateso ambayo ni namna ya mafundisho ya Kiroho na yanapaswa kuonekana kama ushahidi wa Upendo wa Mungu kwetu sisi.

Paulo alitumia nukuu hii kutoka katika Waraka wake kwa Waebrania sura ya 12 mistari ya 5 hadi 13. Hoja aliyoitoa katika Waraka ule imeelezwa vizuri zaidi katika Waraka wake wa pili kwa Wakorintho sura ya 12 mistari ya 7 hadi 10. Paulo, mtume aliyechaguliwa kwa Mataifa, mtu ambaye zaidi ya mara moja alipokea moja kwa moja ufunuo wa Yesu alimwelekeza na kumsaidia, alikuwa na ulemavu wa kudumu kiasi kwamba ulimsumbua na hivyo aliomba kwa Mungu mara tatu ili kuponywa. Paulo katika hoja yake aliweza kupata jibu kutoka kwa Mungu – mstati wa 9. "Neema yangu yakutosha, maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu". Ni wazi kwamba Paulo aliyakubali maneno haya kutoka kwa Mungu na kuendelea na kazi yake ya kusafiri na kuhubiri hadi siku alipokuwa mfungwa wa Warumi.

Pia hatuna budi kujifunza somo lile kutoka katika maneno ya Mungu, udhaifu au mateso ni jambo ambalo tunapaswa kukubali katika maisha yetu. Tusikubali yatuharibie maisha yetu na tusiruhusu kuingilia kumwabudu kwetu Mungu na mwanae, Bwana wetu Yesu Kristo. Hata tunaweza kuelewa mateso kuwa njia ya kupunguza anasa na uharibifu wa dunia inayotuzunguka ili kwamba tukaribie uhusiano wa Mungu na Yesu.

Hakika hii ilikuwa kweli kwa wengi wa Watumishi wa Mungu kutoka Nyakati za Agano la Kale kwa kuwa walijaribiwa sana katika maisha yao hata hivyo imani yao kwa Mungu yaliendelea kuwa na nguvu zaidi kutokana na majaribu hayo. Wengi wao wanaume na wanawake tayari tumekutana nao katika masomo haya na utakumbuka majina yao. Ayubu, Abrahamu, Josefu, Eliya, Danieli na Jeremia ni baadhi tu ya uchaguzi wangu kutoka katika wengi ambao ni mifano kwetu.

Kwa hiyo tumeona kwa makini kuhusu mateso ya mwanadamu na sasa ninataka umfikirie sasa Mungu mwenyewe. Je aliweza kuteseka wakati Israeli watu wateule wake walipomuasi? Je anateseka leo hii kwa ajili ya watu wenye mioyo migumu na kwa ukatili wanaowafanyia wenzao wanaume kwa wanawake?.

Fungua Biblia yako Injili ya Yohana sura y 3 mistari ya 14 hadi 17. Hakika haya ni mateso makubwa sana ambayo angeruhusu mwanaye wa pekee kupigwa na hatimaye kifo kwa kusulibiwa msalabani ili dhambi za binadamu zisamehewe ili wanaume na wanawake wenye imani waweze kuwa na tumaini la uhakika la ufufuo na uzima wa milele.

Yesu alikuja katika asili ya binadamu, alishiriki asili yetu ya udhaifu na kustahimili majaribu yaliyompata na mateso yote yaliyo ya kawaida kwa wanadamu wote.

Maisha haya ya kawaida, aliishi kwa ajili yetu, yamefafanuliwa katika Waebrania sura ya 2 mistari ya 10 hadi 18. Hapa tunapata fundisho muhimu. Yesu "alikamilishwa kupitia mateso" mstari wa 10, ili aweze kuwasaidia wote wanaojaribiwa, mstari wa 18. Katika Waraka kwa Waebrania sura ya 5 mstari wa 8 tunasoma kuwa Yesu alijifunza kutii kutokana na mateso yaliyompata.

Kuteswa kwa ajili ya Mungu ikiwa, kwa kumtii Baba, Yesu alivumilia, matatizo yote ambayo ni maisha ya mwanadamu yanafanyika upya. Pasipo imani tunapoteswa kwa ajili ya Mungu ni kuendelea kuishi maisha ya dhambi. Kwa imani na kupitia mfano wa Yesu aliotuwekea, ni dhahiri kuwa njia ya mateso imani yetu husafishwa (hutakasika). Inawezekana Mungu akaleta mateso kwa mwanafunzi ili iwe njia ya mwanafunzi kunyenyekea. Bwana anapoturudi ieleweke kuwa ni njia ya Uungu katika kufundisha. Tunapoadhibiwa tushukuru na tumwabudu Mungu; kama tumeteseka katika maisha yetu na tukastahimili na kuzidi kumkaribia Mungu ieleweke kuwa hata yeye aliteseka na hupenda tupate nguvu kupitia uzoefu wetu.

CBM Publishing, 32 Blenheim Rd, Far Cotton, Northampton NN4 8NW United Kingdom
PO Box 2950, Mbeya, Tanzania (East Africa)